BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Pili – Tarehe 11 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

87. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Tunaipongeza Serikali kwa kutoa fursa za uwekezaji nchini, hali iliyoongeza vijana wetu kujiajiri na kuajiriwa katika sekta mbali mbali za ajira. Hata hivyo, kumeongezeka malalamiko ya kimasilahi na mikataba isiyoeleweka kwa watumishi hasa wa taasisi binafsi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kikosi kazi kitakachopitia mikataba ya ajira ya watumishi wa sekta binafsi na kuwapa elimu stahiki ya haki zao.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

62. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa juhudi inazozichukua katika kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo kwa njia mbali mbali ili na wao waweze kuyamudu maisha yao. Pamoja na juhudi zinazochukuliwa, bado hadhi ya wafanyabiashara hao inaonekana kukabiliwa na vikwazo mbali mbali.

(a) Je, juhudi za Serikali za kuwatambua mama lishe na wafanyabiashara wengine wadogo wadogo hapa Zanzibar zimefikia hatua ipi ya utekelezaji wake.

(b) Je, kuwatambua huko kunawasaidia vipi katika kuwapunguzia kodi na tozo mbali mbali katika biashara zao wanazozifanya katika maeneo mbali mbali hapa Zanzibar.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

17. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kama tunavyoelewa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa na nchi mbili huru.

Je, ni kwa kiasi gani Zanzibar inanufaika na fedha zinazotoka kwa wafadhili na wahisani mbali mbali kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

7. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Pamoja na jitihada kubwa za makampuni ya simu katika kuleta huduma za simu za mkononi hapa nchini, bado kuna maeneo mengi Zanzibar, ambapo huduma hii imekuwa adimu au isiyo ya uhakika:

   (a) Je, ni ipi hali halisi (status) ya upatikanaji wa huduma ya mitandao ya simu za mkononi (coverage) kwa Zanzibar.

   (b) Je, ni lini Serikali imeyaelekeza makampuni ya simu za mkononi yanayowekeza Zanzibar kukamilisha mitandao yao ili kuwafikia wananchi wote wa Zanzibar mijini na vijijini.

   (c) Je, umefikia wapi mpango wa kuviwezesha vitengo vya kibiashara vya kiserikali kutumia Mkonga hadi kwenye nyumba “Fiber to the Home (FTTH)”.

**Wizara ya Afya:**

3. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

   Kituo cha Afya cha Kiembesamaki na Shakani vipo katika hali hatarishi kwa wagonjwa na wauguzi.

   Je, ni ipi ahadi ya Serikali ya kuvikarabati vituo hivyo ili kuweza kutoa huduma nzuri na salama za kiafya kwa wananchi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

64 MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

   Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa nia nzuri ya kukuza kipato cha wajasiriamali wanaojihusisha na uvuvi kupitia bahari.

   Je, ni lini wajasiriamali wa jimbo la Nungwi watapata mgao wa boti kwa ajili ya kukuza kipato chao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

10. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Zanzibar tumekuwa tukipokea miongo tofauti ya mvua licha ya kupotea kwa utaratibu tuliouzoea wa mvua hizo, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

    (a) Ni lini Serikali itavuna na kuyahifadhi maji ya mvua, ili yaweze kutumika katika shughuli mbali mbali za mzunguko wa maisha yetu.

    (b) Ni changamoto gani zinazopelekea kukwamisha mpango huu na matokeo yake kuyaacha maji ya mvua yakituama katika maeneo yasiyo sahihi kwa matumizi.

    (c) Je, mpango huu wa kuvuna maji ya mvua unaweza ukawa na faida gani katika Mfumo wa Umwagiliaji Maji (Irrigation System).

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

49. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), unatarajiwa pamoja na manufaa mengine, kukinufaisha Chuo Cha Ufundi Karume (KIST) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Mradi huu ni muhimu sana utasaidia kwa kiasi fulani kupunguza changamoto ya kuwa na wahitimu wengi waliokosa ujuzi.

    (a) Je, thamani ya mradi huu ni kiasi gani kwa upande wa Zanzibar.

    (b) Je, mpaka sasa mradi huu umefikia hatua gani na matarajio ya mafanikio yake ni yepi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

5. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ukiachilia mbali kuwa michezo ni moja ya burudani kwa watu wengi duniani, pia imegeuka kuwa moja ya vyanzo vya ajira vyenye kuleta mapato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Licha ya kuwepo kwa fursa nyingi za kimichezo, bado Serikali yetu haijazitumia vyema fursa hizo wala kuweka mpango mkakati imara wenye nia ya kuinua michezo nchini.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuandaa mitaala ya mafunzo kwa viongozi wa vyama vya michezo, ili kuwawezesha kusimamia na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, uweledi na uwazi.

(b) Je, Serikali imefikia wapi katika suala la Zanzibar kujiunga na kujitegemea katika mashirika ya michezo ya kimataifa kama vile FIFA, ili kuviwezesha vyama vyetu vya michezo kushiriki na kujitangaza kimataifa.

(c) Je, Serikali imefikia wapi katika kuanzisha viwanja vya michezo vya Wilaya (4-in-1).

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

24. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwavutia wawekezaji katika kuwekeza zao la karafuu kwa lengo la kuongeza pato la nchi na wakulima wa zao hilo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2023/2024.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
11 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA